

# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

S.L.P. 35091 ♦ DAR ES SALAAM ♦ TANZANIA



## TAARIFA KWA UMMA

### MAHAFALI YA 50 YA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere-Mlimani, kinapenda kuwataarifu wadau wa Chuo na umma kwa ujumla kuwa kitafanya duru ya kwanza ya **Mahafali ya Hamsini (50) siku ya Ijumaa tarehe 24 Julai 2020** katika Ukumbi wa Mikutano wa Mlimani City kuanzia saa sita na nusu mchana. Duru hii ni kwa minajili ya kutunuku Shahada za Uzamivu, Umahiri na Stashahada za Uzamili, pamoja na Shahada za Awali wakiwemo wahitimu wa kwanza wa Ndaki ya Afya na Sayansi Shirikishi iliyoko Mbeya.

Katika duru hii kutakuwa na jumla ya wahitimu **532**. Kati yao **45** watatunukiwa Shahada ya Uzamivu, **418** Shahada za Umahiri, **19** Stashahada ya Uzamili na **50** Shahada za Awali.

#### Mchanganuo wa wahitimu kwa tuzo husika ni kama ifuatavyo:

TUZO	ME	KE	JUMLA	% KE
Shahada ya Uzamivu	33	12	<b>45</b>	26.7
Shahada ya Umahiri	252	166	<b>418</b>	39.7
Stashahada ya Uzamili	18	1	<b>19</b>	5.3
Shahada ya Awali	32	18	<b>50</b>	36.0
<b>JUMLA</b>	<b>335</b>	<b>197</b>	<b>532</b>	37.0

Aidha, katika sherehe hizi za kuadhimisha mahafali ya hamsini tangu kuanzishwa kwake mwaka 1970, Chuo kitawatambulisha wanataaluma wake mahiri waliokidhi vigezo vya kuendelea kukitumikia Chuo katika wadhifa mpya ulioanzishwa wa Profesa Emeritus.

Uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unawakaribisha wadau wote wa elimu ya juu kuhudhuria mahafali haya muhimu katika historia ya Chuo chetu. Pia mahafali haya yatarushwa mubashara kupitia <https://youtu.be/tu5tZv-BoqA>.

Imetolewa na

Prof. William A. L. Anangisye  
**MAKAMU MKUU WA CHUO**